# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

## CHUO CHA UALIMU NDALA

**CHUO CHA UALIMU DALA**
**S.L.P. 9,**

**NDALA – TABORA.**

**SIMU :+255759804804**
**+255783463099**
**+255784902500**

**Barua Pepe:**
**ndalatc@moe.go.tz**
**ndalatc@gmail.com**

**Tarehe 30.06. 2026**

---








**Kumb. Na. ST/I/VOL. V/316**
Ndugu……………………………,
S. L. P ……………………………,
……………...............................

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA STASHAHADA YA YA UALIMU KATIKA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

**1. UTANGULIZI:**

Napenda kukuarifu kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada kwa "**PRE SERVICE**" na '**INSERVICE'** katika Chuo cha Ualimu Ndala. Uongozi wa chuo unakupongeza kwa kupata nafasi hii, mafunzo ya Stashahada ya Ualimu kwa miaka miwili kwa walimu wanachuo watakaokuwepo muda wote Chuoni, na wale wataosoma kwa njia ya masafa kwa miaka mitatu hadi minne. Chuo kitafunguliwa tarehe 13**.07.2026** na mwisho kuripoti chuoni ni tarehe **24.07.2026** Ukichelewa kuripoti kwa muda uliopewa hapo juu hutapokelewa na nafasi yako atapewa mwombaji mwingine.
Chuo kipo Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora. Kutoka Nzega ni umbali wa kilometa 64 upande wa Kusini kuelekea Tabora, na kutoka Tabora ni umbali wa kilometa 60 Kaskazini kuelekea Nzega. Upo usafiri wa mabasi kwenda Ndala kutoka Tabora, Nzega na Igunga kila siku isipokuwa siku ya Jumapili. Kama utapanda basi/hiace Tabora, panda basi/hiace linaloelekea Ndala au kama utapanda bas/hiacei Nzega, panda basi/hiace linaloelekea Ndala.
Kwa upande wa matibabu ipo hospitali kubwa ya Misheni (R.C) na matibabu ni ya kulipia, hivyo njoo na fedha za kutosha au njoo na kadi ya Bima ya afya kwa ajili ya matibabu yako. Utakapofika chuoni ripoti kwenye Ofisi ya usajili wa Wanachuo mara moja ili uweze kusajiliwa. Dira yetu ni Elimu kwa Manufaa ya Umma, Kauli ya Chuo ni **"NDALA COLLEGE CHAPA KAZI"** "Mvivu hana nafasi Chuoni". Kazi za mikono ni sehemu ya Mafunzo yako. Pia utatakiwa kufaulu masomo yako yote katika mitihani utakayokuwa ukiifanya ukiwa chuoni. Kiwango cha kufaulu mitihani ya kila muhula ni kupata wastani wa alama 50% kwa kila somo, Vinginevyo utasimamishwa kuendelea na Mafunzo. Aidha unatakiwa uhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani na shughuli zingine baada ya masomo.

**2.1 MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA USAJILI .**

a. Njoo na vyeti halisi (**original certificates**) vya kumaliza masomo ya kidato cha IV, VI **(leaving certificate**) na cha taaluma, pamoja na vivuli vyake **(Leaving Certificate, result slip/academic certificate), cheti cha UALIMU kwa waliohitimu Astashahada ya Ualimu**na na cheti cha kuzaliwa.
b. Pima afya yako kabla ya kuja Chuoni. (**Request for medical examination form imeambatanishwa).**
c. Ukiwa na matatizo maalum ya kimaumbile na afya toa taarifa kwa Mwadili wa wanachuo mara moja wakati wa kuripoti.
d. Kama umeoa au kuolewa njoo na vyeti vyako vya ndoa na viwasilishe kwa Msajili wa wanachuo.
e. Utakula chakula cha kawaida kinachotolewa na chuo. Hivyo hakuna chakula maalum kwa wagonjwa (**Special Diet**). Wenye matatizo maalum ya chakula watajitegemea.
f. Utajigharamia nauli ya kwenda na kurudi nyumbani wakati wa likizo.
g. Hutaruhusiwa kutoka nje ya chuo kwa siku za Jumatatu hadi Jumamosi. Utatoka siku ya jumapili tu na siku za sikukuu za Taifa kuanzia saa 8 mchana hadi saa 11 jioni.

h. **Mawasiliano yote kutoka kwa wazazi/mlezi yanayomhusu mwanachuo kama vile msiba/magonjwa yapitie Ofisi ya Mkuu wa chuo.**

## 2.2 MAHITAJI YA USAJILI KWA WANACHUO KWA NJIA YA MASAFA

**a.** Njoo na vyeti halisi (**original certificates**) vya kumaliza masomo ya kidato cha IV, **cheti cha UALIMU,** na cheti cha kuzaliwa.

b.Utajigharamia nauli ya kwenda na kurudi wakati wa Mafunzo ya ana kwa ana.

## 3. ADA KWA WANACHUO WA KAWAIDA NA MASAFA

Ada ya Mafunzo ni T.shs. 250,000/= kwa muhula (Tshs. 450,000/= kwa mwaka). Unaweza kulipa ada ya nusu mwaka T.shs. 250,000/= au ada ya mwaka mzima Tshs. 450,000/=. Aidha ya Chuo ilipwe kupitia control number iliyotolewa na mhasibu wa chuo wasiliana naye kwa namba 0686569613.Hakikisha unaandika majina yako kamili kama yalivyo kwenye cheti chako cha shule Badala ya sahihi au vifupisho vya majina ya mwekaji.

## 4.1 MICHANGO KWA WANACHUO WA KAWAIDA

**Michango mbalimbali ni Tsh. 150,000/=** kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini ilipwe kupitia **Akaunti Na. 51101100010 Benki ya NMB.**

**(Jina la akaunti ni Principal Ndala Teachers' College Self - Reliance)**

| **S/NA** | **AINA YA MICHANGO** | **KIASI(TSHS)** | **MUDA** |
|---|---|---|---|
| 1 | Usajili na Kitambulisho | 20,000/= | Kwa mwaka wa kwanza tu |
| 2 | Serikali ya Wanachuo | 5,000/= | Kwa Mwaka |
| 3 | Huduma ya Kwanza | 10,000/= | Kwa Mwaka |
| 4 | Kukodi godoro | 10,000/= | Kwa Mwaka |
| 5 | Michezo | 30,000/= | Kwa Mwaka |
| 6 | Ukarabati | 25,000/= | Kwa Mwaka |
| 7 | Ulinzi | 30,000/= | Kwa Mwaka |
| 8 | Usafi na Mazingira | 20,000/= | Kwa Mwaka |
| **JUMLA KUU** | | **150,000/=** | |

## 4.2 MICHANGO KWA WANACHUO WA MASAFA

**Michango mbalimbali ni Tsh. 150,000/=** kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini ilipwe kupitia **Akaunti Na. 51101100010 Benki ya NMB.**

**(Jina la akaunti ni Principal Ndala Teachers' College Self - Reliance)**

| **S/NA** | **AINA YA MICHANGO** | **KIASI(TSHS)** | **MUDA** |
|---|---|---|---|
| 1 | Usajili | 20,000/= | Kwa miaka mitatu hadi minne |
| 2 | Serikali ya Wanachuo | 5,000/= | Kwa Mwaka |
| 3 | Huduma ya Kwanza | 10,000/= | Kwa Mwaka |
| 4 | Uendeshaji wa Mafunzo | 40,000/= | Kwa Mwaka |
| 5 | Michezo | 30,000/= | Kwa Mwaka |
| 6 | Ukarabati | 25,000/= | Kwa Mwaka |
| 7 | Usafi na Mazingira | 20,000/= | Kwa Mwaka |
| **JUMLA KUU** | | **150,000/=** | |

## 5.1 SARE YA WANACHUO WA KAWAIDA

**Wanaume**

1. Suruali mbili nyeusi zenye linda ndogo (pleats) mbili upande wa mbele kila upande wa zipu (kitambaa kisiwe na mistari).

**(Angalia mfano hapa chini)**



**Nb: Upana wa suruali chini ni inchi 17.**

2. Koti jeusi
3. Tai ndefu nyeusi
4. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba (gidamu)
5. Mkanda mweusi
6. Mashati mawili ya sare ya chuo rangi ya bluu bahari (Light blue) ya mikono mirefu.
7. Soksi nyeusi/ kijivu

**Wanawake**

1. Sketi mbili (2) nyeusi, kitambaa kizito mshono wa **V** Sketi isiwe fupi ivuke magoti na Isibane,

**(Angali mfano hapa chini**)





2. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba, kisigino kifupi.
3. Soksi nyeupe nzito.
4. Kama utavaa hijab, ifanane na rangi ya shati (blue bahari)
5. Koti jeusi
6. Tai fupi nyeusi

**Sare ya Michezo**

Kila mwanachuo ni mwanamichezo, unapaswa kuwa na vifaa vifuatavyo:

1. Track suit rangi ya bluu bahari (Light Blue)
2. Bukta na fulana rangi ya bluu bahari (Light blue)
3. Viatu vya michezo na soksi ndefu rangi ya bluu nyeusi (Dark blue)

**(Angalia mfano hapa chini)**





**5.2M**

Kila mwanachuo anatakiwa kuwa na fedha za matumizi binafsi na mahitaji madogomadogo ya Chuo kama vile kununua vifaa vya usafi binafsi, matibabu na mahitaji mengine.

## 6.VIFAA VYA MALAZI NA TAALUMA (WANACHUO WA KAWAIDA)

a.Shuka mbili rangi ya pinki (zisiwe na maua)

b.Mto na foronya yenye rangi ya pinki

c.Chandarua ya rangi nyeupe au bluu (3 x 6).

d.Vyombo vya chakula (Sahani,bakuli, kikombe na kijiko)

e.Ndoo kubwa moja na ndoo ndogo moja (kuna shida ya maji)

f.Madaftari makubwa (10) na kalamu za kuandikia za kutosha

g.Mkebe wa Hisabati (Mathematical set)

hRimu moja ya karatasi (A4)

iUfagio wa kufagilia mazingira ya nje

jAje na kiasi cha T.Sh**15,000**/= kwa ajili ya TShirt itakayokuwa Sare ya Chuo.

kAje na kadi ya Bima ya afya au mchango wa Bima ya Afya Tsh. **50,400/=** kwa asiye na kadi ya Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu kwani chuo kipo karibu na Hospitali binafsi.

## MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA AFYA:

Pima afya yako kabla ya kuja Chuoni. (Angalia kiambatisho namba 1 cha Request for medical examination form).

**Kiambatisho Na. 2**

## MAELEKEZO YA SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO KWA WANACHUO WA KAWAIDA

Utapewa semina elekezi kuhusiana na sheria na taratibu za chuo pindi ufikapo chuoni, aidha utapewa fomu ya kujaza kukubaliana na sheria na taratibu za Chuo.

## KANUNI ZA CHUO
## CHUO CHA UALIMU NDALA

Mwalimu, anapaswa kuwa mfano kwa jamii , wanafunzi wake na kwa **JUMUIYA** anamoishi. Maneno yake na matendo yake yote yawe ya mifano inayofaa kuigwa. Chuo cha Ualimu Ndala kina kanuni zinazoongoza na kinaendeshwa kwa kufuata sheria za Wizara na kanuni hizo. Ukikiuka moja ya kanuni hizi hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako ikiwa ni pamoja na adhabu au kuachishwa mafunzo .

## KANUNI ZENYEWE NA HATUA ZAKE ZA KINIDHAMU:

1. Kila mwanachuo ajiheshimu mwenyewe, awaheshimu wenzake, wanakufunzi, wafanyakazi wa chuo na watu wengine anaokutana nao, kinyume cha hapo atapata adhabu kulingana na kosa ikiwa ni pamoja na kachishwa Mafunzo.
2. Ni kosa kwa mwanachuo kwenda nyumbani kwa Mkufunzi au mfanyakazi yeyote pasipo ruhusa maalum. Adhabu itatolewa kwa atakayekiuka utaratibu.
3. Kila mwanachuo sharti awahi wakati wowote anapohitajiwa kama vile mstarini,

   Bwaloni, ukumbini, Darasani, katika kazi za nje, anapotakiwa kwa kengele au ishara nyingine. Kutotekeleza hayo adhabu itatolewa.
4. Unatakiwa kuwa msafi na nadhifu wakati wote unapokuwa chuoni, pamoja na kutunza mazingira yako. Adhabu itatolewa ukifanya kinyume.
5. Ni kosa kwa mwanachuo kuacha kuhudhuria vipindi vya masomo au kutofanyaMitihani kwa visingizio vya dini, mila na siasa. Atakayepatikana atafukuzwa Chuo.

6. Ni kosa kwa mwanachuo kumkaribisha mgeni wake chuoni bila kibali maalum (Wageni wanaruhusiwa kufika siku za Jumapili na siku za Sikukuu). Kinyume cha kanuni hii adhabu itatolewa.
7. Yampasa kila mwanachuo aheshimu kazi ya mikono na kuzalisha mali kwa upeo wa uwezo wake. Adhabu itatolewa kwa mtegaji.
8. Kila mwanachuo anawajibika kujituma katika kutunza na kulinda **MALI YA UMMA NA YA WATU WENGINE**. Adhabu ya kulipia uharibifu itatolewa kwa atakayekosa.
9. WIZI wa aina yoyote, uwe wa fedha, vitu au mitihani ni marufuku. atakayepatikana, atafukuzwa Chuo.
10. Ni marufuku kwa mwanachuo kutembelea majumba ya **STAREHE**, majumba ya kufikia wageni na vilabu vya pombe. Atakaepatikana atafukuzwa Chuo.
11. Ni kosa kwa mwanachuo kuwa mdanganyifu. Atakayepatikana atapata adhabu kulingana na kosa la udanganyifu.
12. Ni marufuku kwa mwanachuo kuatoka nje ya chuo bila ruhusa. atakayepatikana atafukuzwa Chuo.
13. Mwanachuo hatakiwi kuwa mjamzito katika kipindi chote cha mafunzo yako. Vinginevyo atakayepatikana atasimamishwa mafunzo.
14. Ulevi wa pombe, bangi au madawa ya kulevya ni marufuku. Atakayebainika atafukuzwa Chuo.
15. Ni kosa kwa mwanachuo yeyote kuhamisha kitu/kifaa chochote cha chuo au cha mtu mwingine bila ruhusa. Atakayepatikana atakabiliwa na adhabu.
16. Ni marufuku kwa mwanachuo yeyote kulala bweninini kwa ugonjwa au udhuru mwingine wakati wa masomo au kazi za nje bila kibali cha Daktari au Mkufunzi anayehusika. Atakayepatikana atapata adhabu.
17. Hurusiwi kwenda nje ya Chuo bila kuvaa sare ya Chuo.
18. Ni marufuku kwa mwanachuo kujipikia chakula ndani ya bweni wala jikoni bilaruhusa. Atakayepatikana atapata adhabu.
19. Migomo ya aina yoyote hairuhusiwi katika Chuo hiki. Ikitokea wahusika wafukuzwa Chuo.
20. Ni lazima ufaulu mitihani yote kwa wastani wa alama 50%. Ukishindwa kupata wastani huo utarudia mitihani au kurudia mwaka.
21. Ni marufuku kwa mwanachuo kuwa na lugha chafu, lugha ya matusi, kuwa mgovi, kupigana na kufanya kitendo chochote kitakachodhalilisha utu wa mtu. Atakayekiuka atafukuzwa chuo.
22. Ni marufuku kuonesha uhusiano wa kimapenzi kati ya mvulana na msichana. Atakayeonekana atasimamishwa mafunzo ya ualimu.
23. Taa zitazimwa 5:00 kamili usiku hivyo kila mwanachuo anatakiwa kuwa kitandani kwake kimya tayari kwa kulala.
24. **Simu za mikononi haziruhusiwi** kutumika katika vyumba vya madarasa, mitihani, katika mikutano ya chuo, wakati wa kazi za mikono, michezo na katika shughuli zote rasmi za chuo. Ikibainika unatumia simu katika maeneo hayo simu hiyo utanyag'anywa na utapewa adhabu kali au kusimamishwa masomo.

ABINEGO E. NDIKUMWE
MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU NDALA
S.L.P. 9 NDALA - TABORA.

**KIAMBATISHO NA. 3.**

**FOMU YA KUJAZA MAELEZO BINAFSI**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU NDALA**

**TAARIFA YA MWANACHUO**
**(IJAZWE NA MWANACHUO MWENYEWE)**
**MAJINA YAKO**
**KAMILI:**___________________________________________________________
**TAREHE YA KUZALIWA**____________________________________________________
**KIJIJI**____________________**WILAYA**___________________ **MKOA**__________________
**DINI DHEHEBU**___________________________________________________________
**JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI**____________________________________________
**ANUANI YAKE:**____________________________________________________________
**UMEOA/UMEOLEWA:**_______________________________________________________
**KIWANGO CHAKO CHA ELIMU:**_____________________________________________
SHULE YA MSINGI ULIYOSOMEA:____________________________________________
MWAKA ULIOMALIZA ELIMU YA MSINGI: ______________________________________
SHULE YA SEKONDARI ULIYOSOMEA__________________________MWAKA__________
DARAJA ULILOPATA (DIVISION)____________________ ALAMA (POINTS)_____________
MASOMO PAMOJA NA MATOKEO YAKE

| **MASOMO:** | **UFAULU WA ALAMA:** |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

MCHEPUO ULIOSOMEA (SAYANSI, BIASHARA, SANAA, KILIMO)___________________
MATATIZO YA KIAFYA ULIYONAYO:_____________________________________________
MSAADA AMBAO UNGEPENDA UPATE KWA MATATIZO YAKO____________________
_____________________________________________________________________________
MICHEZO UNAYOPENDA KUCHEZA:______________________________________________
UTAALAMU MWINGINE ULIONAO:_______________________________________________

**NDUGU ZAKO WALIOKO NZEGA/TABORA**

| JINA LAKE | UHUSIANO | ANUANI YAKE | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |

**NATHIBITISHA KUWA TAARIFA NILIZOTOA HAPO JUU NI SAHIHI NA ZA UKWELI**

**JINA KAMILI:** **SAINI:** **TAREHE**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
**PART A**:

TO: The Medical Officer,

………………………………………………
………………………………………………
………………………………………………

From: The Principal,
Ndala Teachers’ College,
P. O. Box 9,
**NDALA -TABORA.**
Date: ………………………

**Mr/Miss/Mrs**……………………………………………………………………
(Name in Full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training course. The examination should include the following categories (I –IV) each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnancy (Category IV) will also render a girl ineligible for the course.

(i) (a) Eye-sight(e) Leprosy

(b) Hearing (f) Limbs
(c) Speech (g) Epilepsy
(d) Venereal Diseases

(ii) Neuroses (iii) Other serious diseases (iv) Pregnancy

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

**PART B:**
**MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for a full-time teacher training course.

Eye-sight ……………………………………………………….
Hearing ……………………………………………………… Limbs
…………………………………………………………..
Venereal diseases……………………………………………….
Leprosy ………………………………………………………

Epilepsy……………………………………………………………

Neuroses ………………………………………………………….

Other serious diseases ……………………………………….

Pregnancy ………………………………………………………….

Date …………………………………  Signature ………………………………………..

Station ………………………………  Designation ………………………………………

Official stamp